

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE
SHULE YA SEKONDARI YA KIDEGEMBYE

S.L.P 730,
NJOMBE.

Simu: 0756866468

MZAZI/ MLEZI WA

SHULE YA MSINGI

Ndg;

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA KIDEGEMBYE
MWAKA 2021.

1. UTANGULIZI:

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao mtajwa hapo juu amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ya Kidegembye. Hongera sana!

2. MAZINGIRA YA SHULE:

Shule ipo Kata ya Kidegembye, Kijiji cha Kidegembye, Kitongoji cha Madete. Umbali wa kilometa 37 kutoka Njombe mjini. Ni shule ya mchanganyiko (wavulana na wasichana), ni ya kutwa lakini ina hosteli (mabweni), kwa jinsia zote (wavulana na wasichana).

3. TAREHE YA KURIPOTI/ KUFIKA SHULE

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/ 2021. Mzazi/Mlezi anatakiwa kuhakikisha anamleta mwanafunzi bila kukosa siku ya kufunguliwa shule ili aweze kupokelewa na kuanza masomo mapema bila kuchelewa.

4. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA :

A. Vifaa vya masomo kwa wanafunzi wote:-

- (i) Daftari kubwa (counter book 4 QUIRE) 11.
- (ii) Mkebe wa vifaa vya hisabati.
- (iii) Kamusi ya English-Swahili (dictionary) 1.
- (iv) Kalamu za wino na za risasi za kutosha (@ kuanzia 10) na rula 1.

B. Sare za shule:-

Na	DHUMUNI	WASICHANA	WAVULANA
1	Blauzi/shati 2	Nyeupe mikono mirefu	NyeupeMikono mirefu
2	Skeketi 2	Khaki 1 na Damu yam zee 1	
3	Suruali 2		Khaki 1 na Damu yam zee 1
4	Viatu vyeusi pea 2	Vya ngozi siyo yebo.	Vya kamba, visigino vifupi
5	Soksi pea 2	Rangi nyeupe	Rangi nyeusi
6	Sweta	Rangi ya bluu	Rangi ya bluu
7	Nguo za kazi	t-shirt ya njano na sketi ya kijani	t-sheti ya njano na suruali nyeusi
8	Nguo za michezo	Traki blu bahari (LIGHT BLUE) yenye mikanda myeupe na raba	Traki suti nyeusi yenye mikanda myeupe na raba

5. UJAZAJI WA FOMU:

Kila mwanafunzi anatakiwa kujaza fomu zifuatazo kabla ya kuanza masomo:-

- i. Fomu ya kukubali/kukiri kusoma shule
- ii. Fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi
- iii. Fomu ya kupima afya mwanafunzi

Zingatia; Kila mwanafunzi ahakikishe amepima afya yake na fomu yake imethibitishwa na daktari na kugongwa muhuri (official stamp).


6. SHERIA ZA SHULE:

Nakala ya sheria za shule imeambatanishwa na fomu hii ili mwanafunzi ajue taratibu za shule na makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule.

NB: *Wanafunzi wa kike (wasichana) wote watakaa bwenini tu na si vinginevyo, mzazi/mlezi tambua hilo.*

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana shuleni kwa tarehe iliyopangwa hapo juu.

Ahsante!



DAINES S. CHAMBULIKASI


MAHITAJI MENGINE MUHIMU: Wanafunzi wote wanunuliwe nguo za ndani za kutosha i.e Wasichana **kuanzia 5, kwa wavulana kuanzia 3.**

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII:

- i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni lazima.
- ii. Mahudhurio mazuri darasani na katika shughuli za nje kulingana na ratiba ya shule.
- iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni na asubuhi (preparations) ni lazima.
- iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule pamoja na zile utakazo pewa ni lazima.
- v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu mealekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- vii. Kutunza mali za umma.
- viii. Kuvaa sare wakati wote unapotakiwa
- ix. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

YAFUATAYO NI MAKOSA YANAAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi.
2. Ubakaji.
3. Uasherati na ushoga.
4. Kupiga mtu au Kupigana.
5. Kutoa mimba.
6. Kuo au kuolewa.
7. Kuwa mjamzito/kupata mimba au kusababisha mimba.
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
9. Kudharau bendera ya taifa.
10. Kukataa adhabu kwa makusudi.
11. Kuwa na simu ya mkononi.
12. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, n.k.
13. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu kiujumla.



MKUU WA SHULE

“IJAZWE NA MGANGA MKUU MWENYE SIFA KATIKA HOSPITRALI AU
KITUO CHA AFYA KINACHOTAMBULIKA NA SERIKALI”
PRESIDENT’S OFFICE – RALG

KIDEGEMBYE SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 730,
NJOMBE.
5th DECEMBER, 2016.

To Medical Officer,

.....
.....

Please examine.....as to his/her fitness to pursue secondary education.

- A. Hearing
- B. Eye-Sight
- C. Asthma
- D. Leprosy
- E. Epilepsy
- F. S. T. Ds
- G. Heart Problem
- H. Speech
- I. Limbs
- J. Mental problem
- K. Pregnancy “for girls only”
- L. Any other disease/problem (especially HIV/ AIDs).....
.....
.....
.....

Comments:

Name and SignatureOccupation.....

Date